# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA MIUNDOMBINU, ARDHI NA TEHAMA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**JUNI, 2026**

# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MIUNDOMBINU, ARDHI NA TEHAMA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** Kwanza kabisa, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana leo katika Kikao cha Mkutano wa Tatu wa Baraza la Kumi na Moja, kwa lengo la kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako thabiti, wenye busara na hekima, ambao umeendelea kuuonesha katika kuendesha shughuli za Baraza hili Tukufu. Mwenyezi Mungu azidi kukujalia afya, nguvu na uwezo, wewe pamoja na wasaidizi wako, ili muendelee kuliongoza Baraza hili kwa uadilifu, umakini na weledi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kutumia fursa hii kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, **Dkt. Hussein Ali Mwinyi,** kwa uongozi wake makini, wenye maono na unaozingatia

maslahi ya wananchi wa Zanzibar. Tangu aliposhika dhamana ya kuiongoza nchi yetu, ameendelea kuonesha uwezo mkubwa wa kusimamia maendeleo ya kiuchumi, kuimarisha huduma za kijamii, uimarishaji wa miundombinu ya nchi yetu pamoja na kudumisha amani, umoja na mshikamano wa kitaifa.

**Aidha,** Napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar, **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdalla**, ambaye pia ni Kiongozi Mkuu wa Shughuli za Serikali katika Baraza hili Tukufu, kwa namna anavyoendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa, busara na uzalendo wa hali ya juu. Uongozi wake katika kusimamia shughuli za Serikali ndani ya Baraza umeendelea kuimarisha nidhamu, uwajibikaji na ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Serikali. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu viongozi wetu hawa ili azidi kuwapa afya njema, nguvu, hekima na uongozi bora ili waendelee kuitumikia Zanzibar kwa uadilifu, uzalendo na mafanikio makubwa zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** kadhalika, tunatoa pongezi za dhati kwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, **Mheshimiwa Rahma Kassim Ali,** Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, **Mheshimiwa Salha Mohammed Mwinjuma, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu** pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano wanaoutoa katika kutekeleza majukumu yao ndani ya kamati yetu hasa katika kipindi hiki cha kuipitia Bajeti hii.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza jukumu la msingi kwa mujibu wa Kanuni ya 101(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2024, Kamati ilikaa siku ya tarehe 27 Aprili 2026 kuchambua, kujadili na hatimaye kupitisha mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa mchakato huo, Waheshimiwa wajumbe walionesha umahiri na umakini mkubwa kwa kuijadili bajeti hii na kuibua masuala muhimu ya msingi kwa dhamira ya kuhakikisha kuwa fedha zinazoidhinishwa na Kamati zinatumika kama ilivyokusudiwa. Aidha, juhudi hizo zililenga kuimarisha misingi ya uwajibikaji, uwazi na nidhamu katika matumizi ya fedha za umma kwa maslahi ya taifa.

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuendelea na hotuba hii, kwa ruhusa yako na kwa heshima ya kipekee, naomba nichukue fursa hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu, Ardhi na Tehama pamoja na makatibu wake kama ifuatavyo:

1. Mhe: Mihayo Juma N'hunga - Mwenyekiti
2. Mhe: Mwanaidi Kassim Mussa - M/Mwenyekiti
3. Mhe: Hudhaima Mbarak Tahir - Mjumbe
4. Mhe: Khamis Mohammed Amran - Mjumbe
5. Mhe: Said Ali Mbarouk - Mjumbe
6. Mhe: Prof Omar Fakih Hamad - Mjumbe
7. Mhe: Abdullah Kambotwe Abdullah - Mjumbe
8. Ndg: Rahma Kombo Mgeni - Katibu Msaidizi
9. Ndg: Bakari Makame Haji - Katibu Msaidizi
10. Ndg. Adam Maulid Simai - Afisa Bajeti

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 103 (6) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2024, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Miundombinu, Ardhi na Tehama kuhusu

Maoni ya Kamati kwa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kama ifuatavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imeundwa na mafungu mawili (2) ya kibajeti. Hivyo, kwa mwaka wa fedha 2026/2027 wizara hii itatekeleza kazi zake kupitia mafungu makuu mawili (2) ya kibajeti, ambayo ni Fungu 014 – Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, na Fungu 145 Kamisheni ya Ardhi ambayo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 itatekeleza na kusimamia Programu Kuu 5 na Programu Ndogo 11 zitakazojumuisha shuhuli zote zilizopangwa kufanywa ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027.

## FUNGU 014 – WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

**Mheshimiwa Spika,** Fungu 014 – Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imeundwa na program kuu tatu (3) na program ndogo tano (5), ambapo kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Fungu hili limekadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi Bilioni Tatu (3,000,000,000/-)** na kutumia jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Tatu na Nane, Milioni Hamsini na Saba, Laki Saba na Elfu Kumi (308,057,710,000/-)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuendelea kuwawekea wananchi mazingira bora ya makazi kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ya nyumba, ikiwemo miradi inayotekelezwa na Shirika la Nyumba. Miradi hiyo inalenga kuwapatia wananchi nyumba za kisasa, salama na zenye gharama nafuu, hatua ambayo inachangia kuimarisha ustawi wa jamii pamoja na kuboresha maisha ya wananchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya mipango mizuri ya Wizara, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa Wizara inaingiziwa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kinachostahiki, ili kuiwezesha kutekeleza ipasavyo shughuli na mipango iliyojiwekea kwa mwaka wa fedha husika. Kamati ilibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2025/2026, hadi kufikia mwezi Machi 2026, Wizara haikuingiziwa fedha yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, hali ambayo imeathiri utekelezaji wa baadhi ya shughuli zilizopangwa na kuchelewesha kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

**Mheshimiwa Spika,** programu hii imeundwa na programu ndogo tatu (3) ambazo ni S0101 - Uratibu wa Mipango, S0102 - Sera na Tafiti, S0103 - Utawala na Uendeshaji, na Uratibu wa Shughuli za Wizara Ofisi kuu Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, programu hii imekadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Saba Themanini na Mbili, Laki Nane na Elfu Kumi (4,782,810,000/-)** sawa na **asilimia 1.55** ya bajeti yote ya Wizara. Kupitia programu hii, Wizara inatarajia kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo kufanya tafiti, kupitia sera na sheria mbalimbali, pamoja na kuratibu shughuli za Kamati ya Kudhibiti Ujenzi (DCU), kwa lengo la kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya sekta husika.

## PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA ARDHI

**Mheshimiwa Spika,** programu hii imeundwa na programu ndogo moja (1) ambayo ni S0201 - Usimamizi wa Ardhi. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027,

programu hii imekadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano na Kumi, Laki Tisa na Ishirini Elfu (1,510,920,000/-)** sawa na **asilimia 0.49** ya bajeti yote ya Wizara. Programu hii ya usimamizi wa ardhi inatarajiwa kutekeleza shughuli mbalimbali muhimu ikiwemo kusimamia shughuli za uthamini wa mali, kupitia na kuidhinisha ripoti za uthamini, kutatua migogoro ya ardhi, pamoja na kuratibu na kusimamia shughuli mbalimbali za uendeshaji wa programu hiyo kwa ujumla. Kupitia utekelezaji wa shughuli hizi, programu inalenga kuimarisha usimamizi bora wa ardhi na kuhakikisha matumizi yake yanaendana na sheria, taratibu na maslahi ya wananchi pamoja na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa jitihada zake za kuendelea kushughulikia na kutatua migogoro ya ardhi, pamoja na kuhakikisha kunakuwepo usimamizi mzuri wa shughuli za uthamini wa mali kwa madhumuni mbalimbali ya Sekta ya Umma, biashara na wananchi kwa ujumla. Aidha, Kamati inaipongeza Wizara kupitia Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kwa kuandaa Mwongozo wa Uthamini wa Mali na Malipo ya Fidia Zanzibar wa mwaka 2025, ambao unatarajiwa kusaidia kupunguza changamoto zilizokuwa zikijitokeza katika shughuli za uthamini, hususan uthamini wa fidia.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hayo, Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali upande wa Pemba kwa kuongeza watendaji wenye sifa na uwezo stahiki, kutokana na kuwepo kwa uhaba mkubwa wa watumishi katika ofisi hiyo, hali inayoweza kuathiri ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yake.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MAKAAZI

**Mheshimiwa Spika,** programu hii imeundwa na programu ndogo moja (1) ambayo ni S0301 – Maendeleo ya Makaazi. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, programu hii imekadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Tatu na Moja, Milioni Mia Saba Sitini na Tatu, Laki Tisa na Elfu Themanini (301,763,980,000/-)** sawa na **asilimia 97.95** ya bajeti yote ya Wizara. Programu hii ya Maendeleo ya Makaazi inatarajiwa kuboresha upatikanaji wa nyumba za kisasa na za bei nafuu nchini, kuimarisha upatikanaji wa nyumba hizo pamoja na kuratibu usikilizaji, uratibu wa migogoro ya kodi za upangishaji nyumba pamoja na kusimamia usajili wa miradi ya kondomino.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa jitihada zake za kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanapata makaazi bora, salama na yenye gharama nafuu. Hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuimarisha sekta ya makaazi zinaonesha dhamira ya dhati ya kuboresha ustawi wa wananchi na kuhakikisha upatikanaji wa makazi yenye hadhi kwa jamii mbalimbali.

Vilevile, Kamati inaipongeza Serikali kwa nia na mikakati yake ya kuwawezesha wananchi kumiliki nyumba kupitia utaratibu wa malipo ya muda mrefu, hatua ambayo itasaidia wananchi wengi zaidi kupata fursa ya kumiliki nyumba kwa urahisi na kwa wakati unaofaa. Mfumo huo unatarajiwa kuongeza uwezo wa wananchi wa kipato cha kati na cha chini kumudu gharama za makaazi na hivyo kupunguza changamoto ya makazi kwa wananchi wengi.

Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kufanya tathmini ya bei za nyumba zinazojengwa pamoja na kuangalia uwezo halisi wa wananchi kumudu gharama

hizo, ili kuhakikisha nyumba zinazotolewa zinaendana na hali ya kiuchumi na kipato cha wananchi wengi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya mipango mizuri na mikakati iliyoandaliwa na Wizara katika kutekeleza azma na malengo yake ya maendeleo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa Wizara inapatiwa fedha za kutosha, hususan fedha za miradi ya maendeleo, ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kufikia malengo iliyojiwekea.

Kamati ilibaini kuwa hadi kufikia mwezi Machi 2026, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi haikuingiziwa fedha yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, hali ambayo imeathiri utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo na kuifanya Wizara kushindwa kufikia baadhi ya malengo yake ya kimkakati. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ilikadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Tatu Thelathini na Tano, Milioni Mia Sita Themanini na Tano (335,685,000,000/-)** kwa ajili ya miradi ya maendeleo, hata hivyo hadi kufikia Machi 2026 hakuna fedha yoyote iliyokuwa imeingizwa kwa madhumuni hayo.

Aidha, Kamati imeelezwa kuwa kupitia programu hii, Wizara inatarajia kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo inayolenga kuimarisha sekta ya ardhi na makaazi nchini. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, programu hiyo imepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Tatu, Milioni Mia Tisa na Ishirini (300,920,000,000/-)** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hivyo, Kamati inaona ipo haja kwa Serikali kuhakikisha fedha hizo zinapatikana kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji madhubuti wa mipango na miradi iliyokusudiwa kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

## FUNGU 145 – KAMISHENI YA ARDHI

**Mheshimiwa Spika,** Fungu 145 – Kamisheni ya Ardhi imeundwa na program kuu tatu (2) na program ndogo tano (6), ambapo kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Fungu hili limekadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Mbili na Hamsini, na Laki Mbili (11,250,200,000/-)** na kutumia jumla ya **Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Saba Tisiini na Mbili, Laki Tano na Elfu Mbili (8,792,502,000/-).**

## PROGRAMU KUU YA UPANGAJI NA USIMAMIZI WA ARDHI

**Mheshimiwa Spika,** programu hii imeundwa na programu ndogo nne (4) ambazo ni S0101 – Utawala na Usimamizi wa Ardhi, S0102 – Upimaji na Utayarishaji wa Ramani, S0103 - Uandaaji wa Mipango wa Matumizi ya Ardhi pamoja na S0104 – Usajili wa Ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, programu hii imekadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne na Thelathini na Sita, Laki Tano Ishirini na Sita Elfu (1,436,526,000/-),** sawa na **asilimia 16.33** ya bajeti yote ya Kamisheni ya Ardhi. Kupitia programu hii, Kamisheni inatarajia kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo Utoaji wa huduma za upimaji na utayarishaji wa ramani, Utoaji wa huduma za uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi, Utoaji wa Huduma za usajili wa ardhi pamoja na Utoaji wa huduma za utawala na uendeshaji wa Kamisheni ya Ardhi.

## PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI WA KAMISHENI YA ARDHI

**Mheshimiwa Spika,** programu hii imeundwa na programu ndogo nne (2) ambazo ni S0201 – Uratibu wa Shughuli za Mipango naUtawala, S0202 – Uratibu wa Shughuli za Kamisheni ya Ardhi Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, programu hii imekadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Tatu Hamsini na Tano, Laki Tisa Sabiini na Sita Elfu (7,355,976,000/-)** sawa na **asilimia 83.66** ya bajeti yote ya Kamisheni ya Ardhi. Kupitia programu hii, Kamisheni inatarajia kuendelea kutoa huduma bora za uendeshaji wa shughuli za Kamisheni ya Ardhi kwa upande wa Pemba na Unguja.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa Kamisheni ya Ardhi katika kutekeleza majukumu yake na kuipatia fungu lake la kibajeti, jambo ambalo litawezesha Kamisheni hiyo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, weledi na kwa kujitegemea zaidi katika kusimamia masuala ya ardhi nchini.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia maoni na mapendekezo yaliyotolewa, Kamati inaunga mkono Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2026/2027, huku ikisisitiza umuhimu wa kuyatekeleza kikamilifu mapendekezo hayo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya kipekee, napenda kumshukuru Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Ndg. Raya Issa Mselem, kwa uongozi wake mzuri katika kuwaongoza watumishi wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kwenye uratibu na usimamizi wa shughuli mbalimbali za Baraza hili Tukufu, ikiwemo shughuli za vikao vya Kamati pamoja na maandalizi ya kikao hiki cha Bajeti, ambayo yamefanyika kwa ufanisi na umakini mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liunge mkono hoja kwa kuichangia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuwasilisha.

……………..…………

Mihayo Juma N'hunga,

Mwenyekiti,

Kamati ya Miundombinu, Ardhi na Tehama,

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR.**